

YALIYOMO

UKURASA

Utangulizi.....	2
Kuitambua Miti Dawa.....	2
Ukitaka Upendeke Kwa Watu Wote.....	3
Kubatwilisha Uchawi Uliopo Tumboni.....	3
Dawa Ya Koo Kuwasha.....	4
Dawa Ya Kikohozi.....	4
Dawa Ya Mtu Aliyefunga Choo Kidogo.....	5
Kutibu Vidonda Vya Tumbo.....	5
Kutibu Nguvu Za Kiume.....	6
Kufungua Biashara Iliyofungwa.....	6
Dawa Ya Mwili Kufa Ganzi Au Kuwaka Moto.....	7
Kumrejesha Mlowezi Au Mtu Aliyepotea.....	7
Kutibu Homa Ya Manjano.....	7
Matibabu Ya Mbavu Kubana.....	8
Dawa Ya Kutibu Malaria, Typhoid Na Minyoo.....	8
Tiba La Sikio Linalotoa Taka Au Usaha.....	9
Dawa Ya Kutibu Chango.....	9
Nyungu Ya Kutoa Viumbe Wabaya Mwilini.....	10
Nyungu Ya Magome Kutibu Masheitwani.....	10
Faida Za Mtundwa.....	11
Maradhi Yanayotibiwa Na Mizizi Ya Mtundwa.....	11
Kuondosha Ubaya Na Kuvuta Kheri.....	12
Tiba Ya Jini Mahaba.....	13
Matibabu Ya Hernia.....	14
Kutibu Jino.....	14
Kumfungua Anaachelewa Kujifungua.....	14
Kutibu Ugonjwa Wa Bawasiri.....	15
Kutibu Presha.....	15
Kutibu Macho.....	16
Kutibu Ugonjwa Wa Kupooza Viungo.....	16
Kutibu Homa.....	18
Kutibu Mgongo.....	18
Dawa Zinazotumika Kufunga Hedhi.....	19
Kutibu Donda Ndugu.....	19
Tiba Ya Machango Aina Zote.....	19

UTANGULIZI

Sifa Njema Zote Anastahiki Allah (Subhaanahu Wa Ta'aala) Mola Wa Walimwengu Wote, Rehema Na Amani Zimshukie Kipenzi Chetu Mtume Muhammad (Swalla Allahu 'Alayhi Wa Aalihi Wa Sallam) Na Swahaba Zake (Radhiya Allahu 'Anhum) Na Waliowafuata Kwa Wema Mpaka Siku Ya Mwisho.

Tunamshukuru Mola Wetu Mlezi Kwa Kutuwezesha Kuandaa Kitabu Hiki Chenye Anuani Ya “Uponyaji Kwa Dawa Za Miti”.

Kitabu Hiki Kimelenga Kuifahamisha Jamii Juu Ya Majina Na Namna Ya Kutumia Dawa Za Miti Kuondosha Na Kuponya Matatizo Mbalimbali Yanayo Muandama Mwanadamu.

KUITAMBUA MITI YA DAWA

Ni Jambo La Muhimu Kwa Kila Mtu Anayetaka Kutumia Dawa Za Miti Au Kuotesha Kwa Ajili Ya Biashara, Aweze Kuitambua Sawasawa Miti Ya Madawa Ambayo Anataka Kutumia Au Kupanda Shambani Kwake.

Njia Bora Ni Kutembelea Mahali Ilipooteshwa Au Pale Ilipojiotea Yenyewe Na Uangalie Kwa Umakini Jinsi Ilivyo; Angalia Umbo Lake Na Rangi Za Maua Yake, Angalia Majani Na Mbegu Zake, Nusa Harufu Yake, Pia Onja Utamu Wake.

Madawa Ya Mimea Mara Nyingi Yana Ladha Yake Maalum; Chungu, Tamu, Au Chachu. Na Harufu Yake Maalum Pia; Harufu Nzuri Au Mbaya Kutokana Na Vitu Vilivyomo Katika Mmea Au Mti Dawa Husika.

Tahadhari; Usije Ukala Mti Au Mmea Ambao Haufahamiki Na Kamwe Usije Ukameza Maji Au Utomvu Wa Mmea Ambao Huna Mazoea Nao; Inawezekana Mmea Huo Una Sumu.

UKITAKA UPENDEKE KWA WATU WOTE

MAHITAJI;

Mwinamo

Mvuto

Mkoma Vikali

Nyota

Mpendwapendwa

MATUMIZI;

Changanya Dawa Hizo Zote Pamoja Na Mafuta Ya Nazi.

Tumia Kwa Kujipaka Kila Unapotoka.

KUBATWILISHA UCHAWI ULIOPO TUMBONI

MAHITAJI;

Mwingajini

Mhunungu

Msokonowe

Mkumbi

Mtimkuu

Altiti

Mjafari

Mkokoma

Katakwa

MATUMIZI;

Changanya Dawa Hizo Zote Kwa Pamoja.

Pima Kijiko Kidogo Cha Chai Na Uchemshe maji robo lita, kunywa ya vuguvugu.

Tumia Kutwa Mara Mbili (Asubuhi Na Jioni) Siku Saba